

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA AFYA

TANGAZO LA NAFASI ZA WAHUDUMU WA AFYA NGAZI YA JAMII

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia **Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI)** inatekeleza **Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii** nchini. Kupitia Mpango huu, Serikali imeweka utaratibu wa kuwapata Wahudumu wenye sifa zilizowekwa, kutoa mafunzo na kuwatumia Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii katika utekelezaji wa afua Jumuishi za Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii ambapo Mpango unahitaji Wahudumu wawili (2) yaani Mwanaume na Mwanamke kwa kila Kitongoji/Mtaa.

Katika kutekeleza Mpango huu, **Wizara ya Afya** kwa kushirikiana na **Ofisi ya Rais - TAMISEMI** inawatangazia Wananchi kuwa **Mpango huu kwa awamu ya kwanza utaanza katika Mikoa 10 na Halmashauri mbili (2) kwa kila Mkoa** kama inavyoonekana katika Jedwali:

MKOA	NA	HALMASHAURI	IDADI YA WAHUDUMU (CHWS)
GEITA	1	Geita TC	224
	2	Bukombe DC	696
		Jumla	920
KAGERA	1	Bukoba MC	132
	2	Biharamulo DC	746
		Jumla	878
KIGOMA	1	Buhigwe DC	384
	2	Kakonko DC	710
		Jumla	1094
LINDI	1	Lindi MC	234
	2	Lindi/Mtama DC	1490
		Jumla	1724
MBEYA	1	Mbeya CC	362
	2	Busokelo DC	474

		Jumla	836
NJOMBE	1	Makambako TC	242
	2	Njombe TC	504
		Jumla	746
PWANI	1	Kibaha TC	146
	2	Rufiji DC	334
		Jumla	480
SONGWE	1	Tunduma TC	142
	2	Ileje DC	632
		Jumla	774
TABORA	1	Tabora MC	586
	2	Nzegha TC	380
		Jumla	966
TANGA	1	Handeni TC	120
	2	Tanga City Councils	362
		Jumla	482
		JUMLA KUU	8,900

Aidha, Utekelezaji wa Mpango huu utaendelea kwa awamu katika Mikoa na Halmashauri zote za Tanzania Bara. Wananchi wenye sifa stahiki ndani ya Mikoa 10 iliyooneshwa katika Jedwali hapo awali, **wanahimizwa kuomba nafasi za Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii katika Mitaa/Vitongoji vyote ndani ya Halmashauri zao. Maombi yote yawasilishwe kwa Wakurugenzi waHalmashauri**, ambao watasimamia zoezi la kuwachagua Wahudumu wenye sifa miongoni mwa waliotuma maombi kwa kuzingatia Miongozo iliyotolewa.

Sifa za waombaji:

- a) Awe na utambulisho rasmi kama vile Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au Hati ya kusafiria au Leseni ya Udereva au Kitambulisho cha Mpiga Kura;
- b) Awe amemaliza Elimu ya Sekondari (angalau Kidato cha Nne) na awe na Cheti cha Kuhitimu (*Leaving Certificate*);
- c) Awe ni mkazi na kwa sasa anaishi Kitongoji/Kijiji na Mtaa husika;
- d) Awe anafahamu lugha, utamaduni, mila na desturi za Jamii husika;
- e) Akubalike Kimaadili na Kiutamaduni na jamii husika;

- f) Asiwe na historia ya vitendo vya uhalifu ikiwemo unyanyasaji wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto;
- g) Awe na moyo wa kujituma, mchapakazi na mwenye ari ya kutumikia jamii;
- h) Awe mwaminifu na mwenye uwezo wa kuweka taarifa za mteja kuwa siri;
- i) Awe na utayari na uwezo wa kufanya kazi katika Kitongoji au Mtaa husika na;
- j) Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 55.

Maombi yawasilishwe Ofisi ya Mtendaji wa Kata yakiambatanishwa na:

- a) Barua ya maombi ya kazi iliyoandikwa kwa mkono na kuwekwa saini ya mwombaji
- b) Nakala ya Cheti cha kuhitimu Kidato cha Nne (*Form IV Leaving Certificate*);
- c) Picha mbili (2) za *Passport Size*;
- d) Maelezo binafsi (CV), ikionyesha umri, anuani kamili na namba ya simu ya kiganjani, pamoja na anuani/namba ya simu ya kiganjani ya Wadhamini wasiopungua wawili (2).
- e) Barua ya uthibitisho kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa wa eneo analotoka.

Mwisho wa kuwasilisha maombi haya ni **wiki mbili (2)** tangu tarehe ya kutolewa kwa tangazo hili. Maelekezo zaidi yanapatikana kupitia **Ofisi za Watendaji wa Kata** husika.

Imetolewa na:

KATIBU MKUU
S.L.P 743 DODOMA
06/04/2024